**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**

# TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA NISHATI (FUNGU 58) KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

---

*[Imetolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]*

**DODOMA** **MEI, 2023**

# YALIYOMO

**YALIYOMO**......i
**VIELELEZO** ...... iii
**VIFUPISHO VYA MANENO** ......iv
**SEHEMU YA KWANZA**...... 1
**1.0 UTANGULIZI**...... 1
1.1 Msingi na Muundo wa uchambuzi wa Bajeti ...... 2
**SEHEMU YA PILI** ...... 3
**2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA UZINGATIAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ...... 3**
2.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo...... 3
2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo...... 4
2.2.1 Miradi ya REA Wilaya ya Korogwe...... 4
2.2.2 Mradi wa Ujenzi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi – ni...... 6
2.2.3 Mradi wa ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme cha Chalinze (Namba ya Mradi 3272)...... 7
2.2.4 Mradi wa upanuzi wa Kituo cha kuzalisha umeme cha Kinyerezi I - *Kinyerezi I Extension MW 185* (Namba ya Mradi 3164) ...... 8
2.2.5 Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya usambazaji wa Gesi Asilia katika Mkoa wa Dar Es Salaam, Lindi na Pwani na Kituo cha kupokelea Gesi Asilia cha Kinyerezi (GASCO) (Namba ya Mradi 3162) ...... 10
2.3 Tathmini ya Miradi...... 12
2.4 Maoni, Ushauri na Mapendekezo...... 13
2.5 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023...... 15
2.6 Uchambuzi wa Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Februari 2023...... 16
2.7 Uchambuzi wa Upatikanaji wa Fedha kufikia Februari 2023 ...... 17
2.8 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati...... 19
**SEHEMU YA TATU** ...... 20
**3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024** ...... 20
3.1 Uchambuzi wa Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024...... 20
3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024...... 21
3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024...... 22
3.4 Ulinganisho baina ya Bajeti ya Wizara na Bajeti ya Taifa...... 25
3.5 Uchambuzi wa Masuala Mahsusi...... 27
3.5.1 Hali ya Upatikanaji wa Umeme Nchini...... 27

3.5.2 Hali ya Mafuta Nchini ........ 28
**SEHEMU YA NNE** ........ 33
**4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** ........ 33
4.1 Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania (TANESCO) ........ 33
4.2 Wakala wa Umeme Vijijini –REA ........ 34
4.3 Shirika la Maendeleo la Petroli (TPDC) ........ 35
4.4 Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli - PURA ........ 36
4.5 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ........ 36
4.6 Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) ........ 37
4.7 Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania - TGDC ........ 37
**SEHEMU YA TANO** ........ 38
5.0 **HITIMISHO** ........ 38

# VIELELEZO

**Kielelezo Na. 1** : Upatikanaji wa Fedha kwa Miradi iliyotembelewa ................. 12
**Kielelezo Na. 2** : Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Februari, 2023 ........................ 16
**Kielelezo Na.** : Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida ..................... 17
**Kielelezo Na. 4** : Upatikanaji wa Fedha za Maendeleo kufikia Februari, 2023 .................................................................................... 18
**Kielelezo Na. 5** : Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli 2022/2023 na 2023/2024............................................................ 22
**Kielelezo Na.** : Mgawanyo wa Bajeti kwa Mwaka 2023/2024 ........................ 23
**Kielelezo Na. 8** : Maeneo ambayo Bajeti imeongezeka.................................... 24
**Kielelezo Na. 9(a)** : Ulinganisho wa Bajeti (Fungu 58) dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 .......................................... 25
**Kielelezo Na 9(b)** : Ulinganisho wa Bajeti (Fungu 58) dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 .......................................... 26
**Kielelezo Na. 10** : Hali ya Uzalishaji wa Umeme Nchini…………………………..27
**Kielelezo Na. 11** : Kiasi cha mafuta kilichoingizwa Nchini………………………30

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| CCM | Chama cha Mapinduzi |
| CNOOC | China National Offshore Oil Corporation |
| EWURA | Energy and Water Utilities Regulatory Authority |
| FYDPIII | Third National Five Years Development Plan |
| JNHPP | Julius Nyerere Hydropower Project |
| LNG | Liquified Natural Gas |
| LPG | Liquefied Petroleum Gas |
| MPSA | Model Production Sharing Agreement |
| MVA | Megavolt Amperes |
| OC | Other Charges |
| PBPA | Petroleum Bulk Procurement Agency |
| PE | Personal Emolument |
| PURA | Petroleum Upstream Regulatory Authority |
| REA | Rural Energy Agency |
| SDG's | Sustainable Development Goals |
| SLA | Service Level Agreement |
| TANESCO | Tanzania Electric Supply Company Limited |
| TANOIL | TANOIL Investment Limited |
| TBS | Tanzania Bureau of Standards |
| TGDC | Tanzania Geothermal Development Company Limited |
| TIPPER | Tanzania International Petroleum Reserves Limited |
| TPDC | Tanzania Petroleum Development Corporation |
| UNOC | Uganda National Oil Company |
| VETA | Vocational Education and Training Authority |

## TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA NISHATI (FUNGU 58) KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023[1], nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Wizara ya Nishati **(Fungu 58)** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**.**

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya Kamati kuhusu Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara inazozisimamia ikiwemo bajeti ya Wizara hii yameelezwa kwa kina katika fasili ya 7(1) (a) ya nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023[2].

**Mheshimiwa Spika**, Uandishi wa Taarifa hii umezingatia matakwa ya Kanuni ya 123 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023 kama ifuatavyo:-

a) Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi na inaeleza kuhusu Msingi na Muundo wa Taarifa;

---

[1]118 (9) Baada ya Waziri kuwasilisha Hotuba ya Bajeti kwa mujibu wa fasili (1), Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Makadirio husika na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni watatoa maoni yao kwa muda usiozidi dakika thelathini kila mmoja.

[2] 7.-(1) Majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge za kisekta yatakuwa yafuatayo:- (a) kushughulikia bajeti ya Wizara inazozisimamia;

b) Sehemu ya Pili inaeleza kuhusu uchambuzi wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na namna Wizara ilivyotekeleza Ushauri na Mapendekezo ya Kamati;

c) Sehemu ya Tatu inachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

d) Sehemu ya Nne inatoa Ushauri na Mapendekezo yake kwa Wizara na Serikali kwa ujumla; na

e) Sehemu ya Tano ambayo ni ya mwisho ni Hitimisho la Taarifa yenye kujumuisha shukrani na kutoa hoja.

## 1.1 Msingi na Muundo wa uchambuzi wa Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023, inazitaka Kamati zote za Kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuchambua Taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia na kufanya ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa fedha unaofuata[3].

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia matakwa haya ya Kanuni za Bunge, Kamati ya Nishati na Madini kuanzia tarehe 23 -27 Machi, 2023 ilitekeleza wajibu wake kwa kufanya uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Nishati yenye fungu moja 58.

[3] Baada ya kutembelea miradi, Kamati za Bunge za Kisekta, kwa kipindi kisichozidi siku tisa, zitafanya vikao vya kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoisha na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata

## *SEHEMU YA PILI*

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA UZINGATIAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Kamati katika uchambuzi wake kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ilijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

a) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2022/2023;

b) Uchambuzi wa utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati;

c) Uchambuzi wa utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

d) Uchambuzi wa hatua iliyofikiwa katika ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na

e) Uchambuzi wa Upatikanaji wa fedha kufikia Februari 2023.

### 2.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023[4], kabla ya kuanza uchambuzi wa bajeti, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Nishati. Kamati ilifanya Ziara katika Mikoa mitatu (3) ambayo ni Tanga, Pwani na Dar es Salaam ili kuona hatua iliyofikiwa katika

[4] 117(1) Baada ya kuwasilishwa kwa mapendekezo ya mpango na kiwango cha ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata kwa Wabunge, Kamati za Bunge za kisekta zitatembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha, kwa siku zisizozidi saba.

utekelezaji wa miradi hiyo. Aidha, ziara ililenga pia kubainisha mafanikio na changamoto ili kuweza kulishauri Bunge lako Tukufu na Serikali hatua za kuchukua.

## 2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia ziara hiyo, yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi wa miradi iliyotembelewa na Kamati:-

### 2.2.1 Miradi ya REA Wilaya ya Korogwe

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu wa Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (Lot 39) katika Wilaya ya Pangani, Korogwe na Mkinga unatekelezwa na Mkandarasi M/s Tontan Project Technology and Group Six International Ltd wenye lengo la kupeleka umeme katika **vijiji 79** kwa gharama ya **Shilingi 22,815,588,709.89/=**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Wilaya ya Korogwe ambapo Kamati ilitembelea, Mradi unahusisha kusambaza umeme katika vijiji 54; ujenzi wa njia za umeme wa msongo wa kati zenye urefu wa kilomita 253; ujenzi wa njia za umeme wa msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 54; ufungwaji wa mashine umba 54 pamoja na uunganishaji wa wateja wa awali 1,188. Mradi ni wa miezi 18 na ulianza kutekelezwa rasmi tarehe 14 Februari 2022 na unatarajiwa kukamilishwa mwezi Agosti 2023. Gharama za Mradi ni **Shilingi 12,496,697,661.284 (Pamoja na VAT)**. Mpaka sasa kiasi cha **Shilingi 2,499,339,532.26** zimekwisha lipwa sawa na **asilimia 20** ya gharama za mradi.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi huu umekuwa unasuasua kwani mkandarasi amesimamisha nguzo za njia ya msongo wa kati urefu wa kilomita **30 kati ya 253,** amesimamisha nguzo za njia ya msongo mdogo urefu wa

kilomita **7 kati ya 54**, amejenga mtandao wa umeme wa njia ya msongo wa kati wenye urefu wa **kilomita 20** kati ya **253** alizopewa kwenye mkataba; amejenga **kilomita 4** kati ya **54** za njia za msongo mdogo, amefunga mashine umba **4** kati ya **54** na ameunganisha umeme kwa wateja wa awali **40** kati ya **1,800** sawa na **asilimia 11.**

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na maelezo kuwa kuongezeka kwa bei ya vifaa kumesababisha mradi huu kuchelewa, hata hivyo, pamoja na kupitia upya gharama ya bei za vifaa, Mkandarasi kuandikiwa barua na kufanya nae kikao bado mkandarasi yupo nyuma ukilinganisha na mkataba. Kamati ilikutana na Mkandarasi na ilipomuhoji sababu za kuchelewa kutekeleza mradi alikiri ni kweli alipewa fedha kiasi cha **Shilingi Bilioni 3.86** kwa ajili ya kutekeleza Mradi (Lot 39) katika Wilaya ya Pangani, Korogwe na Mkinga na fedha hizo alizitumia kwa shughuli nyingine. **Kamati imesikitishwa sana na kitendo cha Mkandarasi kutumia fedha za Umma kwa shughuli zake nyingine. Kitendo hiki kimeihuzunisha sana Kamati. Si hivyo tu, lakini pia Kamati haipendezwi na kasi ndogo ya utekelezaji wa Mradi huu ambao ni mfano kati ya mingi nchini. Maeneo mengi utekelezaji wa miradi hii umekuwa wa kusuasua kutokana na kutowajibika ipasavyo kwa baadhi ya Wakandarasi. Ni rai ya Kamati kwa Watendaji wa Serikali kuongeza umakini katika kutoa zabuni kwa Wakandarasi na kusimamia kwa karibu utekelezaji wa miradi hii.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata nafasi ya kutembelea na kushuhudia uwashaji wa umeme katika vijiji viwili vya Mswaha Darajani ambapo umeme uliwashwa katika Shule ya Msingi, Msikiti na Kijiji cha Madumu umeme uliwashwa katika Shule ya Sekondari ya Chekelei.

### 2.2.2 Mradi wa Ujenzi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi – Chongoleani

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu ambao unahusisha ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi (*crude oil*) kutoka Hoima-Kabaale nchini Uganda hadi Chongoleani -Tanga nchini Tanzania likiwa na urefu wa kilomita 1,443. Kati ya hizo, kilomita 296 zitakua Uganda na kilomita 1,147 zitapita Tanzania. Kwa upande wa Tanzania bomba litapita katika Mikoa 8 na Wilaya 24. Gharama ya mradi ni **Dola za Kimarekani Bilioni 5.088** ambazo zinajumuisha fedha za wanahisa Total energies (62%), TPDC (15%), UNOC (15%) na CNOOC (8%). Hadi kufikia Februari 2023, kiasi cha **Dola za Kimarekani Milioni 891.85** zilikuwa zimetolewa kama mchango wa kila mwanahisa kwa mujibu wa hisa zake na utekelezaji wa mradi huu ni wa kipindi cha miezi 36.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali ilitenga kiasi cha **Shilingi Bilioni 5.5.** kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu. Kufikia mwezi Februari 2023, kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.8** kilikuwa kimetolewa sawa na **asilimia 53** ya fedha zote. Upatikanaji wa fedha hizo umewezesha kuanza utekelezaji wa hatua mbalimbali za mradi. Baadhi ya kazi ambazo Kamati imeelezwa na nyingine kushuhudia ni pamoja na utwaaji wa ardhi kwa **asilimia 98**, kusafishwa kwa eneo la mradi lenye kujumuisha maeneo mbalimbali kama eneo la kupokelea matenki ya mafuta ghafi na gati, kuanza kwa ujenzi wa Kempu ambao umefikia **asilimia 20** na inatarajiwa kukamilika mwezi huu wa Mei 2023, na kuchimbwa kwa mabwawa kwa ajili ya kupokea maji endapo mvua itatokea ili kutoathiri eneo la ujenzi.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi una jumla ya Wafanyakazi 400 ambapo Wageni 50 na Watanzania 350. Kati ya Watanzania hao 150 wanatoka katika eneo la mradi (Chongoleani). Aidha, utekelezaji wa mradi huu unaenda sambamba na miradi mingine ya kimazingira na kijamii kama kujenga uwezo kwa wananchi, ujenzi wa barabara na kufundisha Watanzania 170 katika Vyuo vya VETA na Chuo cha Ufundi Arusha ambao watafanya kazi katika Mradi na tayari 40 wameshahitimu. Aidha, kwa miezi sita ijayo mpango ni kukamilisha ujenzi wa Kempu, barabara, na kuondoa udongo ambao kwa sasa upo **asilimia 40** na kuanza msingi wa matenki.

### 2.2.3 Mradi wa ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme cha Chalinze (Namba ya Mradi 3272)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi wa kusafirisha umeme kutoka Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) hadi Chalinze na kituo cha kupoza umeme cha Chalinze. Utekelezaji wa Mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni: Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 kutoka JNHPP hadi Chalinze yenye urefu wa kilomita 160; na Ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Chalinze, ambacho kinahusisha ufungaji wa mashine umba (transfoma) sita zenye uwezo wa MVA 250 kila moja.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia 100 ambazo ni **Dola za Kimarekani milioni 51.5 na Shilingi bilioni 39.12** kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na **Dola za Kimarekani milioni 44.06** na **Shilingi bilioni 30.85** kwa ajili ya kituo cha kupoza umeme cha Chalinze. Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Bunge liliidhinisha **Shilingi Bilioni 40** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu na kufikia Februari 2023 kiasi cha

**Shilingi Bilioni 27.6** sawa na **asilimia 69** kilikuwa kimepokelewa. **Kamati inapongeza mwenendo wa upatikanaji wa fedha.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilishuhudia na kuelezwa kuwa, utekelezaji wa njia ya kusafirisha umeme katika msongo wa kilovoti 400 kutoka JNHPP hadi Chalinze (kilomita 160) umefikia **asilimia 92** na kituo cha kupoza umeme cha Chalinze, ambacho kinahusisha ufungaji wa mashine umba (*transfoma*) sita zenye uwezo wa MVA 250 kila moja umefikia **asilimia 59. Kamati inapongeza hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, ujenzi wa Jengo la kuongoza mitambo umefikia wastani wa asilimia 25 na hivyo kuna umuhimu wa kuongeza kasi. Ni imani ya Kamati kuwa, mradi huu utakamilika mapema ili kuweza kupokea umeme kutoka katika Bwawa kama ambavyo Kamati ilihakikishiwa kufikia Juni 2023, Kituo kitakuwa na uwezo wa kupokea umeme kutoka Julius Nyerere kiasi cha MW 235 kutokana na kufungwa kwa mashine umba ya kwanza.**

### 2.2.4 Mradi wa upanuzi wa Kituo cha kuzalisha umeme cha Kinyerezi I - *Kinyerezi I Extension MW 185* (Namba ya Mradi 3164)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Kinyerezi *I Extension* - **MW 185** ambao ulibuniwa ili kuongeza uwezo na upanuzi wa kituo cha Kinyerezi I chenye uwezo wa kufua umeme wa **MW 150**. Lengo ni kuimarisha na kuongeza uwezo wa gridi ya Taifa na kufanya jumla ya uwezo wa kituo cha Kinyerezi I kuwa **MW 335**. Mradi unahusisha usimikaji wa mitambo minne (4) ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi (*gas turbines*), vipoza hewa (chillers) sita (6) pamoja na viambata vyake na tayari vifaa vyote vimeshafika eneo la mradi. Aidha, mradi unahusisha kazi ya kuongeza uwezo wa

njia ya kusafirisha umeme (*transmission line upgrade*) inayotoka Kinyerezi hadi Gongolamboto yenye msongo wa kilovoti 132.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi umefikia **asilimia 93.2** na Kamati ilishuhudia mitambo mitatu kati ya minne (Na. 5, 6 na 7) ikiwa imewashwa na kuingiza **MW 135** kwenye gridi ya Taifa. Wakati Kamati inatembelea mradi, mkandarasi alikuwa anaendelea na kazi ya kuunganisha mtambo wa nne na wa mwisho kwa mradi huu na Kamati ililezwa kuwa mtambo huu ungewashwa mwishoni mwa mwezi April. Kamati pia ilishuhudia ujenzi wa Tenki la maji ukiendelea.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi unagharimiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100 kwa kiasi cha **Dola za Marekani milioni 188** sawa na takriban **Shilingi za Kitanzania Bilioni 435.48** na kiasi cha **Dola za Marekani Milioni 154** kimeshalipwa sawa na **asilimia 82** ya gharama za mradi. Katika Mwaka huu wa fedha 2022/2023 kiasi cha **Shilingi Bilioni 35** kiliidhinishwa na Bunge na kufikia Februari 2023 **Shilingi Bilioni 29.32** sawa na **asilimia 84** zilikuwa zimepokelewa. Kwa ujumla hali ya upatikanaji wa fedha inaridhisha. **Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, mradi huu ni moja ya miradi ambayo utekelezaji wake umechelewa. Itakumbukwa kuwa, awali mitambo yote ilipaswa kuwa imewashwa mwezi Agosti 2022, hata hivyo baadae Kamati ilielezwa ingewashwa mwezi Disemba 2022. Mpaka Kamati inatembelea Mradi huu bado mtambo mmoja (Na. 8) ulikuwa bado haujawashwa**. **Kamati inaitaka Wizara isimamie vizuri mradi huu ili mtambo wa nne uwashwe kama ulivyopangwa ili kuongeza upatikanaji wa umeme nchini.**

### 2.2.5 Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya usambazaji wa Gesi Asilia katika Mkoa wa Dar Es Salaam, Lindi na Pwani na Kituo cha kupokelea Gesi Asilia cha Kinyerezi (GASCO) (Namba ya Mradi 3162)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi huu wa miundombinu ya usambazaji wa gesi katika Kituo cha kupokelea gesi cha Kinyerezi Dar es Salaam. Mradi huu unahusisha mitambo ya kuchakata gesi asilia iliyopo Madimba mkoani Mtwara na Songo Songo Mkoani Lindi; Bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Madimba na Songo Songo hadi Tegeta, Dar es Salaam; na mtandao wa usambazaji gesi kwa watumiaji wa mwisho. Kazi zote za uendeshaji na matengenezo ya miundombinu ya Taifa ya gesi asilia zinafanywa na wataalamu wa GASCO kwa asilimia 100.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla uchakataji wa gesi ghafi unafanyika katika mitambo miwili iliyopo Madimba mkoani Mtwara na Songo Songo mkoani Lindi, ambayo hupokea gesi ghafi kutoka kwa wazalishaji wa mkondo wa juu (*Upstream Operators*). Gesi asilia iliyochakatwa husafirishwa hadi Dar es Salaam kupitia bomba kuu la kusafirisha gesi asilia. Mitambo ya Madimba na Songo Songo kwa pamoja ina uwezo wa kuchakata futi za ujazo milioni 350 (Madimba 210 na Songo Songo 140) kwa siku. Kwa sasa matumizi ya gesi asilia yameongezeka na kiasi cha wastani wa futi za ujazo milioni 105 kinachakatwa kwa siku (105mmscfd).

**Mheshimiwa Spika**, Bomba la kusafirisha gesi asilia kwa ujumla lina urefu wa kilomita 551 kutoka Mtwara na Songo Songo hadi Tegeta, Dar es Salaam. Bomba lina uwezo wa kusafirisha gesi futi za ujazo milioni 784 kwa siku (784mmscfd) bila mgandamizo, na linaweza kusafirisha gesi kiasi cha futi za ujazo milioni 1,002 kwa kuweka mitambo ya mgandamizo

(*compression*). Kwa sasa usafirishaji kwa siku ni wastani wa futi za ujazo milioni 107 -155 sawa na wastani wa **asilimia 20** ya uwezo wa bomba.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia, GASCO inatekeleza mradi wenye urefu wa Kilometa 15.3 na kuunganisha nyumba 125 na taasisi 4 (Sekondari ya Ufundi, Chuo cha Ualimu Ufundi, Chuo cha Ualimu kawaida na Gereza la Lilungu) kwa matumizi ya gesi asilia Mtwara, Mradi wa kuunganisha gesi katika kiwanda cha Rady-Mkuranga kwa urefu mita 802, mradi wa ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia yenye urefu wa Kilometa 4.3 na kuunganisha nyumba 85 (Mikocheni), miradi ya ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia yenye urefu wa Kilometa 16.4 na kuunganisha nyumba 155 na taasisi 2 (Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam).

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka huu wa fedha 2022/2023, **Shilingi Bilioni 1.048** zilitengwa na kufikia Februari 2023 **Shilingi Milioni 891** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 85** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kamati ilitembelea na kuona namna Kituo cha kupokelea gesi cha Kinyerezi kinavyoendeshwa ikiwa ni pamoja na kutembelea Kituo cha kupunguza mgandamizo wa gesi (*Pressure Reduction Station*) na Kituo cha kuangalia usalama wa bomba (*Control Center*). **Kwa ujumla kazi inaenda vizuri isipokuwa Kamati imebaini kuwa kasi ya uunganishwaji wa nyumba/viwanda/taasisi kwajili ya matumizi ya gesi upo chini na haiendani na nia ya Serikali ya kuhakikisha gesi inakuwa ni mkombozi kwa Watanzania. Aidha, uzalishaji wa gesi ni mdogo na hivyo kufanya hata bomba pamoja na ukubwa wake kusafirisha gesi kidogo kutokana na uzalishaji mdogo. Kuna umuhimu wa kuongeza uzalishaji wa gesi ili kukidhi mahitaji ya soko. Mwanasiasa Bill Richardson kutoka Marekani ambaye aliwahi kuwa Gavana**

**wa New Mexico amewahi kusema “*Natural Gas is future, it is here*”. Ni wakati sasa wa kutumia gesi hii ipasavyo.**


**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi nzuri inayofanywa na GASCO, Kamati ilielezwa uwepo wa changamoto zifuatazo:-

i) Ukosefu wa Bodi;
ii) Upungufu wa Wafanyakazi; na
iii) Deni kubwa inalolidai TANESCO kutokana na uuzaji wa gesi kiasi cha **Shilingi Bilioni 725.**

## 2.3 Tathmini ya Miradi

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla kasi ya utekelezaji wa miradi siyo wa kuridhisha kama ilivyoelezwa na zaidi kwa Mradi wa REA Wilaya ya Korogwe ambao umefikia **asilimia 11** tu. Wastani wa upatikanaji wa fedha kwa miradi iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati ni **asilimia 85.1** kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 1.**

**Kielelezo Na. 1: Upatikanaji wa Fedha kwa Miradi iliyotembelewa**




*Chanzo: Taarifa ya Wizara ya Nishati na usanifu wa Kamati*

## 2.4 Maoni, Ushauri na Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia ziara hiyo na yale yaliyobainika, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo:-

**2.4.1** Kutokana na changamoto ya Wakandarasi kushindwa kutekeleza miradi kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za ukosefu wa fedha:-

a) Kabla ya Wakandarasi wa REA kupewa Mikataba ya kazi, uchunguzi wa kina (*Due diligence)* ufanyike ili kuufahamu undani wao ili kuepuka usumbufu katika utekelezaji wa miradi;

b) Mkakati wa Serikali wa kutaka kuwasaidia Wakandarasi wa nje kwa kuwapatia dhamana (*Letter of Credit* - LC) ujielekeze kwa Wakandarasi wazawa ambao ni wazalendo ili kuwainua;

c) Vipengele vya Mkataba na Kampuni ya Tontan inayotekeleza Mradi wa Lot 39 viangaliwe na hatua kali zichukuliwe ili iwe fundisho kwa Wakandarasi wengine ambao wamekuwa wakisuasua kukamilisha miradi licha ya kupewa fedha; na

d) Kwa Wakandarasi wazawa ambao wanatekeleza kazi zao vizuri ni vyema wakazingatiwa na kupewa kazi ambazo Wakandarasi wa nje wameshindwa kuzitekeleza kwa wakati.

**2.4.2** Kutokana na baadhi ya Miradi ya TANESCO kuchelewa kwasababu ya kufilisika kwa wakandarasi:-

a) Uchunguzi wa kina *(Due diligence)* ufanyike kwa Wakandarasi wa nje ili kuepuka kukwama kwa miradi

kunakotokana na maelezo kuwa Wakandarasi wamefilisika;

b) Wakandarasi wadogo (*Subcontractors)* ambao wengi ni wazawa wawe wanalipwa kwanza pale mkandarasi anaposema amefilisika kupitia *Performance Guarantee Bond* kwani wengi wamekuwa hawalipwi;

c) Wakandarasi wa ndani ambao ni waaminifu haswa kwa miradi ambayo inatekelezwa kwa fedha za ndani wapewe kipaumbele cha zabuni;

d) Mamlaka zinazohusika na ununuzi na utoaji wa zabuni zisimamiwe ili kufanya kazi kwa weledi na uadilifu; na

e) Kutokana na uwepo wa changamoto ya upatikanaji wa vifaa zikiwemo nguzo, Wizara ihakikishe vifaa vyote zikiwemo nguzo za kutosha zinapatikana ili utekelezaji wa miradi usikwame.

**2.4.3** Kutokana na kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi mingi ya TANESCO ukiwemo Mradi wa Kinyerezi I Extension, TANESCO inapaswa iwekeze katika usimamizi wa miradi yake *(Project Management*) ili iwe inakamilika kwa wakati na hivyo kuongeza uzalishaji wa umeme nchini. Aidha, TANESCO ihakikishe inasimamia kikamilifu utekelezaji wa Mradi wa *Kinyerezi I Extension* wa MW 185 ili Mtambo uliobaki ukamilike mapema na kuongeza upatikanaji wa umeme nchini.

**2.4.4** TPDC iongeze kasi ya kuunganisha gesi kwa ajili ya matumizi ya majumbani na kwenye Taasisi. Aidha, Sekta Binafsi ishirikishwe ili kuleta ufanisi hususan katika kusambaza gesi ya kutumia kwenye magari ( *Compressed Natural Gas*);

**2.4.5** Wizara isimamie kikamiilifu ili ujenzi wa mradi wa Bomba la mafuta uende kwa kasi; na

**2.4.6** Wizara iendelee kutoa elimu kwa jamii hususan kwa wananchi wa maeneo ya Mkuza wa Bomba kuhusu umuhimu wa kutunza mradi na kuwa walinzi.

## 2.5 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Vipaumbele vya Serikali kwa ujumla vinapaswa kuzingatia masuala mbalimbali kama vile Dira ya Maendeleo ya Taifa, Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa CCM na zaidi Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III), 2021/22 – 2025/26. Wizara ya Nishati ambayo ndiyo imepewa dhamana ya kusimamia Sekta ya Nishati nayo inapaswa kuzingatia haya ilikufikia malengo yaliyowekwa na Katiba yetu ibara ya 8 (1) (b) ya kuhakikisha ustawi wa wananchi[5].

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara umebaini kuwa, Wizara imejitahidi kutekeleza vipaumbele vyake vya kuzingatia Mpango huo wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III), 2021/22 – 2025/26. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, baadhi ya vipaumbele hususan Kipaumbele Na.2 kinachohusu kutekeleza miradi ya umeme vijijini siyo cha kuridhisha kutokana na utekelezaji wake kusuasua kama ambayo imeonekana katika mradi uliotembelewa katika Wilaya ya Korogwe. **Ni Rai ya Kamati kuwa, changamoto zilizobainishwa na Kamati zifanyiwe kazi ili kuboresha ustawi wa wananchi**.


[5] 8 (1) Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii, na kwa hiyo ((b) lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi;

## 2.6 Uchambuzi wa Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Februari 2023

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ilikadiria kukusanya **Shilingi 20,393,000/=** kutoka vyanzo vyake vitatu ambayo ni Marejesho ya Fedha za Umma (*Recovery of Public Money*) kwa **asilimia 99.99** na **asilimia 0.01** kutokana na Stakabadhi nyinginezo na Stakabadhi za aina mbalimbali. Kufikia Februari 2023, Wizara imefanikiwa kukusanya **Shilingi 4,438,259/=** sawa na **asilimia 22** tu ya lengo kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 2.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, chanzo hiki mara kwa mara kimekuwa hakifikii malengo inayojiwekea. Kamati ilhoji sababu za kutofikia malengo na ilielezwa ni kutokana na ukweli kuwa chanzo hiki kinategemea marejesho ya fedha za umma zitokanazo na masurufu (*imprest)* ambayo Watumishi hupewa na kufanya marejesho, hivyo basi kutokana na usimamizi thabiti wa marejesho na baadhi ya watumishi waliokuwa wanakatwa masurufu kumaliza makato yao, makusanyo ndiyo hayo. Kamati inaona ipo haja ya kupunguza Makadirio haya ili kuwa na uhalisia.

**Kielelezo Na. 2: Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Februari, 2023**




*Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara 2023 na Usanifu wa Kamati*

## 2.7 Uchambuzi wa Upatikanaji wa Fedha kufikia Februari 2023

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, Wizara ya Nishati (**Fungu 58**)iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu **Shilingi 2,905,981,533,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Fedha hizo zinajumuisha Matumizi ya Kawaida **Shilingi 82,951,957,000/=** sawa na **asilimia 2.9** ya fedha yote ambapo **Shilingi 14,726,136,000/=** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi (P.E) na **Shilingi 68,225,821,000/=** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) ya Wizara. Aidha, Miradi ya Maendeleo iliidhinishiwa **Shilingi 2,823,029,576,000/=** sawa na **asilimia 97.1** ya fedha zote ambazo zinajumuisha fedha za ndani **Shilingi 2,655,556,128,000/=** na fedha za nje **Shilingi 167,473,448,000/=.**

**Mheshimiwa Spika**, kufikia Februari 2023, Wizara imepokea **Shilingi 1,546,042,818,494/=** sawa na **asilimia 52.6** ya bajeti yote iliyoidhinishwa. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kuwa, kati ya fedha zilizopokelewa Mishahara ni **Shilingi 9,583,074,764/=** sawa **na asilimia 65.08** na Matumizi Mengineyo **Shilingi 7,459,102,675/=** sawa na **asilimia 10.93** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na.3**.

**Kielelezo Na. 3: Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida**





*Chanzo: Taarifa ya utekelezaji ya Wizara na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini pia kuwa, fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi 1,550,392,616,642/=** sawa na **asilimia 66** ya bajeti iliyoidhinishwa ambazo ni fedha za ndani**.** Kwa upande wa fedha kutoka nje, Kamati ilielezwa kuwa kiasi cha **Shilingi 66,757,312,555.62** sawa na **asilimia 39.8** ya bajeti ya maendeleo kutoka nje kimepokelewa kwa utaratibu wa D-Fund ambao hesabu zake huingizwa kwenye Hesabu za Wizara baada ya Mwaka wa Fedha kukamilika. **Kamati bado hairidhishwi na upatikanaji wa fedha kutoka nje.**

**Mheshimiwa Spika**, **Kielelezo Na.4**. kinaonesha hali ya upatikanaji wa fedha kufikia Februari 2023

**Kielelezo Na. 4: Upatikanaji wa Fedha za Maendeleo kufikia Februari, 2023**




*Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara na Usanifu wa Kamati*

## 2.8 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 iliyowasilishwa Bungeni mnamo tarehe 1 Juni, 2022 pamoja na mambo mengine, ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yapatayo 35 ili yafanyiwe kazi na Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** katika kikao cha Kamati kilichofanyika tarehe 23 Machi 2023, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo hayo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwa kiasi kikubwa Wizara imejitahidi kutekeleza maoni, ushauri na mapendekezo hayo ya Kamati. Aidha, kwa baadhi ya hoja ambazo zilikuwa bado hazijatekelezwa kikamilifu, Kamati iliomba ufafanuzi na majibu ya Wizara yalionesha nia ya Serikali katika kuyatekeleza. Kamati itaendelea kusisitiza tena hoja hizo ambazo bado katika Taarifa hii. **Ni Rai ya Kamati kuwa, utekelezaji wa Mapendekezo na Ushauri huo uende kwa kasi ili kusaidia kuimarisha Sekta ya Nishati kama ilivyoainishwa katika Aya ya 63 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 inayosema "*Katika miaka mitano ijayo, Chama cha Mapinduzi kinakusudia kuimarisha zaidi sekta ya nishati kwa kuhakikisha kuwa nchi inazalisha umeme wa kutosha ili kukidhi mahitaji ya uchumi wa viwanda na soko la nje".***

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

a) Uchambuzi wa Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

b) Uchambuzi wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

c) Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

d) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024; na

e) Uchambuzi wa Masuala Mahsusi.

### 3.1 Uchambuzi wa Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati kuhusu Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Nishati (Fungu 58) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 umebaini kuwa, malengo na vipaumbele vya Wizara vimezingatia miongozo mbalimbali ukiwemo Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III), 2021/22 – 2025/26. Aidha, malengo haya yamezingatia dhima ya utekelezaji wa

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) inayosema **"Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu"** ambapo pamoja na mambo mengine bajeti ya Wizara itajumuisha utekelezaji wa miradi ya kipaumbele kama Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere na Miradi ya REA.

**Mheshimiwa Spika**, malengo ambayo Wizara imepanga kuyatekeleza katika Mwaka ujao wa fedha 2023/2024 na ambayo pia yameelezwa kwa kina na Waziri mwenye dhamana ni pamoja na :-

a) Kuongeza uzalishaji na kuboresha mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme;
b) Kuongeza mchango wa nishati jadidifu na mbadala katika matumizi mbalimbali ya nishati;
c) Kuimarisha na kuendeleza matumizi bora ya nishati;
d) Kuimarisha uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za mafuta na gesi asilia;
e) Kuimarisha usambazaji na matumizi ya bidhaa za mafuta na gesi asilia;
f) Kuimarisha utoaji huduma kwa wadau wa Sekta ya Nishati;
g) Kutekeleza kwa ufanisi Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Kuzuia Rushwa; na
h) Kupunguza maambukizi ya VVU na UKIMWI sehemu za kazi na kuboresha utoaji wa huduma kwa waathirika.

## 3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Nishati(Fungu 58)imekadaria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 20,393,000/=.** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio haya yanafanana na yale yaliyokadiriwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na.5. Hata hivyo, Kamati inapata mashaka na makadirio ya makusanyo haya**

**kutokana na kukosa uhalisia. Itakumbukwa kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 makusanyo kufikia Februari 2022 yalikuwa ni asilimia 28 tu. Aidha, katika Mwaka huu wa Fedha 2022/2023 makusanyo kufikia Februari 2023 nayo yalikuwa ni asilimia 21.7 tu ya lengo. Kamati inaona ni vyema makadirio haya yawe na uhalisia.**

**Kielelezo Na. 5: Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli 2022/2023 na 2023/2024**

| CHANZO | 2022/2023 | 2023/2024 | ONGEZEKO/ UPUNGUFU | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| **Marejesho ya Fedha za Umma (Recovery of Public Money)** | 20,391,000 | 20,391,000 | - | - |
| **Stakabadhi nyinginezo** | 1,000 | 1,000 | - | - |
| **Stakabadhi za aina mbalimbali** | 1,000 | 1,000 | - | - |
| **JUMLA** | **20,393,000** | **20,393,000** | **-** | **-** |

*Chanzo: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati*


### 3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia malengo na vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Nishati yenye Fungu 58, inakadiria kutumia **Shilingi 3,048,632,519,000/=** . Fedha hizi zinajumuisha Fedha za Maendeleo **Shilingi 2,960,702,821,000/=** sawa na **asilimia 97.1** ya bajeti yote na **Shilingi 87,929,698,000/=** sawa na **asilimia 2.9** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha za Miradi ya Maendeleo, **Shilingi 2,609,156,128,000/=** sawa na **asilimia 88.1** ni fedha za ndani na **Shilingi 351,546,693,000/=** sawa na **asilimia 11.9** ni fedha za nje. Aidha, kwa upande wa fedha za Matumizi ya Kawaida

zinajumuisha Mishahara ya Watumishi (PE) ambayo ni **Shilingi 16,292,586,000/=** sawa na **asilimia 18.5** na Matumizi Mengineyo (OC) **Shilingi 71,637,112,000/=** sawa na **asilimia 81.5**. **Kielelezo Na. 6** kinachanganua mgawanyo huo wa bajeti.

**Kielelezo Na. 6: Mgawanyo wa Bajeti kwa Mwaka 2023/2024**





*Chanzo: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake, Kamati pia imelinganisha bajeti ya Fungu 58 kwa Mwaka 2022/2023 na 2023/2024 na kubaini kuwa, Bajeti ya Wizara imeongezeka kutoka **Shilingi 2,905,981,533,000** Mwaka 2022/2023 hadi kufikia **Shilingi 3,048,632,519,000** ambayo ni ongezeko la **Shilingi 142,650,986,000** sawa na **asilimia 4.9. Kamati inapongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Wizara hii.**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kuwa, ongezeko zaidi linaonekana katika Miradi ya Maendeleo na hususan fedha kutoka nje kwa **asilimia 109.9**. Aidha maeneo mengine ambayo bajeti imeongezeka ni pamoja na Mishahara (PE) **asilimia 10.6** na OC **asilimia 5**. Vilevile, Kamati imebaini fedha za Miradi ya Maendeleo ndani zimepungua kwa **asilimia 1.7** kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na.7**.

**Kielelezo Na. 7: Ulinganisho wa Bajeti 2022/2023 na 2023/2024**




*Chanzo: Taarifa za Wizara na usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilihoji sababu za ongezeko la fedha za maendeleo kutoka nje na uhakika wa upatikanaji wake hasa ikizingatiwa kuwa katika Mwaka wa fedha 2022/2023 hadi kufikia Februari 2023 wakati Kamati inapokea Taarifa, upatikanaji wa fedha hizo ulikuwa ni **asilimia 39.86 tu.** Kamati ilihakikishiwa kuwa fedha hizo zitapatikana. Kwa ujumla, maeneo ambayo yamepewa kipaumbele katika ongezeko la bajeti ya Wizara kwa Mwaka huu 2023/2024 ni kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 8.**

**Kielelezo Na. 8: Maeneo ambayo Bajeti imeongezeka**

| Na. | Eneo | Sababu |
|---|---|---|
| **1.** | Mishahara | Ajira Mpya, kupandishwa vyeo na Nyongeza ya Mishahara |
| **2.** | Matumizi Mengineyo | Ongezeko la Posho ya Kujikimu kutokana na Waraka wa Watumishi wa Umma Na. 1 wa Mwaka 2022 |
| **3.** | Maendeleo Nje | Kuongezeka kwa fedha za miradi kama ya REA, Rusumo, Kakonko, Malagarasi na North West Grid Extension |

*Chanzo: Taarifa ya Wizara na Usanifu wa Kamati*

### 3.4 Ulinganisho baina ya Bajeti ya Wizara na Bajeti ya Taifa

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati ulienda mbali zaidi kwa kulinganisha Bajeti ya Wizara hii na Bajeti ya Taifa. Ulinganisho uliangalia bajeti ya Wizara kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024 dhidi ya bajeti ya Taifa kwa kipindi hicho. Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa masuala mbalimbali yafuatayo:-

a) Bajeti ya Wizara kwa ujumla dhidi ya Bajeti ya Taifa imeshuka kutoka **asilimia 7.01** Mwaka 2022/2023 hadi **asilimia 6.87** Mwaka 2023/2024.


b) Bajeti ya Matumizi Mengineyo ya Wizara dhidi ya bajeti ya Taifa ya Matumizi mengineyo imeshuka kutoka **asilimia 0.90** Mwaka 2022/2023 kufikia **asilimia 0.66** Mwaka 2023/2024**.**

c) Bajeti ya Wizara ya Maendeleo dhidi ya bajeti ya Taifa ya Maendeleo ndani imeongezeka kutoka **asilimia 21.58** Mwaka 2022/2023 hadi kufikia **asilimia 21.97** Mwaka 2023/2024.

d) Bajeti ya Wizara ya Maendeleo nje dhidi ya bajeti ya Taifa ya Maendeleo nje imeongezeka kutoka **asilimia 6.20** Mwaka 2022/2023 hadi kufikia **asilimia 10.71** Mwaka 2023/2024.

**Kielelezo Na. 9(a): Ulinganisho wa Bajeti (Fungu 58) dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

| BAJETI YA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2022/2023 | | | |
|---|---|---|---|
| **AINA** | **BAJETI TAIFA** | **BAJETI NISHATI** | **ASILIMIA** |
| **OC** | 4,493,500,000,000.00 | 68,225,821,000.00 | 1.52 |
| **MISHAHARA** | 9,740,800,000,000.00 | 14,726,136,000.00 | 0.15 |
| **MAENDELEO NDANI** | 12,122,100,000,000 | 2,655,556,128,000 | 21.91 |
| **MAENDELEO NJE** | 3,399,200,000,000 | 167,473,448,000 | 4.93 |
| **DENI LA SERIKALI** | 11,308,400,000,000.00 | | - |
| **JUMLA** | **41,064,000,000,000.00** | **2,905,981,533,000.00** | **7.08** |




**Kielelezo Na 9(b): Ulinganisho wa Bajeti (Fungu 58) dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

| BAJETI YA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2023/2024 | | | |
|---|---|---|---|
| **AINA** | **BAJETI TAIFA** | **BAJETI NISHATI** | **ASILIMIA** |
| **OC** | 5,578,433,000,000 | 71,637,112,000.00 | 1.28 |
| **MISHAHARA** | 10,882,126,000,000 | 16,292,586,000 | 0.15 |
| **MAENDELEO NDANI** | 11,873,900,000,000 | 2,609,156,128,000 | 21.97 |
| **MAENDELEO NJE** | 3,282,100,000,000 | 351,546,693,000 | 10.71 |
| **DENI LA SERIKALI** | 12,771,500,000,000 | 0 | - |
| **JUMLA** | **44,388,059,000,000.00** | **3,048,632,519,000.00** | **6.87** |




*Chanzo: Taarifa ya Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024 na Randama ya Wizara ya Nishati 2023/2024*

### 3.5 Uchambuzi wa Masuala Mahsusi

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uchambuzi wa Bajeti, Kamati imefanya uchambuzi wa masuala mahsusi ambayo yana maslahi kwa Taifa. Masuala hayo ni Hali ya uzalishaji wa umeme na Hali ya Mafuta nchini kama ifuatavyo:-

#### 3.5.1 Hali ya Upatikanaji wa Umeme nchini

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Nishati ina jukumu la kuhakikisha kuwa wakati wote uzalishaji wa umeme, na uimarishaji wa miundombinu ya kusafirishia umeme nchini unakuwa wa uhakika. Hata hivyo, pamoja na malengo hayo, hali ya umeme bado siyo ya kuridhisha kutokana na umeme kuwa unakatika mara kwa mara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kufikia mwezi Februari, 2023 uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa ulikuwa MW 1,822.05 unaozalishwa kutoka vyanzo vinne Maji MW 574.60, (31.54%), Gesi asilia MW 1,148.82 (63.05%), Mafuta MW 88.13 (4.84%) na Tungamotaka MW 10.50 (0.58%) kama inavyooneka kwenye **Kielelezo Na.10.**

**Kielelezo Na. 10: Hali ya Uzalishaji wa Umeme Nchini**




*Chanzo: Taarifa ya TANESCO na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba uzalishaji wa umeme ambao umeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa ni **MW 1,822.05** sawa na ongezeko la **asilimia 7.52** ikilinganishwa na **MW 1,694.55** zilizokuwepo kufikia mwezi Juni 2022 ni dhahiri kuwa ongezeko la **MW 127.5** ni dogo sana kuweza kuhimili kasi ya ongezeko la mahitaji ya umeme nchini hasa ikizingatiwa kua ukuaji wa shughuli za kiuchumi umekua mkubwa. Aidha, ongezeko hili dogo linaiweka nchi kwenye hatari ya kutoweza kuhimili changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza kwenye mitambo ya kuzalisha na kusambazia umeme. Changamoto hizo ni pamoja na kuharibika kwa baadhi ya mitambo, kushuka kwa kiwango cha uzalishaji wa Gesi, na kushuka kwa kiwango cha maji kwenye mabwawa ya kuzalishia umeme na hivyo kulazimika kusitisha uzalishaji wa umeme. Ni kutokana na kuwepo kwa mazingira haya tunajikuta kwenye mazingira ya kuwa na umeme usio wa uhakika ambao unakatika mara kwa mara na hivyo kuleta athari kwenye uchumi wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, **Kamati inaendelea kusisitiza umuhimu wa Taifa letu kuwekeza zaidi rasilimali fedha kwenye sekta hii ili kuweza kuongeza na kuboresha miundombinu ya kuzalisha na kusambaza umeme. Kwani kwa kufanya hivyo tutaweza kujihakikishia kuwa na umeme wa kutosha na halikadhalika kuondokana na changamoto ya umeme kukatika mara kwa mara. Sambamba na hilo, ipo haja vilevile ya kuimarisha usimamizi wa miradi, na kuongeza kasi ya kukamilisha miradi ya kuzalisha umeme ambayo inaendelea nchini kwasasa hususan mradi wa kimkakati wa Bwawa la Julius Nyerere.**

### 3.5.2 Hali ya Mafuta Nchini

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa majukumu ya Wizara ya Nishati ni kuimarisha usambazaji na matumizi ya bidhaa za mafuta na Gesi asilia nchini. Kwa upande wa mafuta, jukumu


hili limeelekezwa kwa kwa Wakala wa Uagizaji wa mafuta kwa pamoja (PBPA). Majukumu mengine ya Wakala ni pamoja na kutathmini mahitaji ya mafuta nchini na kuratibu uagizaji wa mafuta hayo kwa Mfumo wa manunuzi ya pamoja (*Bulk Procurement System* – BPS). Vile vile Wakala umepewa jukumu la kuhakikisha mafuta yanayoletwa nchini yanakidhi mahitaji na ubora unaotakiwa na kuhakikisha mafuta yananunuliwa kwa njia yenye ufanisi (*efficient procurement*) kwa manufaa ya Taifa, na kuhakikisha kunakuwepo na uhakika wa usalama wa upatikanaji wa mafuta nchini (*Security of Supply*).

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati kuhusiana na hali ya upatikanaji wa mafuta nchini umebaini uwepo wa akiba ya mafuta inayokidhi mahitaji ya nchi. Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai 2022 hadi Februari 2023 akiba ya Mafuta nchini imeendelea kuwa juu ya wastani wa siku za matumizi kwa zaidi ya siku 25 ikiwa ni zaidi ya asilimia 35 ikilinganishwa na siku 15 za akiba ya mafuta inayotakiwa kuwepo kulingana matakwa ya Leseni ya biashara ya jumla ya mafuta.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Februari, 2023, jumla ya **Tani 4,263,245** za mafuta ya dizeli, petroli, ndege na taa ziliingizwa kwa matumizi ya ndani ya nchi (*local*) na nchi za jirani (*transit*) kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 11**. Katika kiasi hiki cha mafuta, jumla ya **tani 1,939,836** sawa na **asilimia 45.5** kilikuwa kwa ajili ya matumizi ya ndani, na **tani 2,323,410** sawa na **asilimia 54.2** kwa ajili ya nchi za jirani.

**Kielelezo Na. 11: Kiasi cha Mafuta kilichoingizwa nchini**

| MWEZI | PETROLI | MAFUTA YA TAA/NDEGE | JUMLA |
|---|---|---|---|
| Jul-22 | 232,365 | 26,884 | 684,828 |
| Aug-22 | 213,164 | 37,890 | 662,747 |
| Sep-22 | 222,123 | 26,830 | 687,926 |
| Oct-22 | 215,680 | 32,162 | 626,128 |
| Nov-22 | 12,720 | 26,660 | 317,275 |
| Dec-22 | 135,944 | 28,861 | 413,244 |
| Jan-23 | 141,340 | 15,500 | 410,126 |
| Feb-23 | 157,931 | 26,025 | 460,974 |
| **JUMLA** | **1,331,267** | **220,812** | **4,263,248** |




*Chanzo: Taarifa ya PBPA na usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** tangu kuanza kutumika kwa mfumo wa Uagizaji Mafuta Kwapamoja (BPS), mfumo umekua ukiimarika siku hadi siku na kuendelea kuaminika na nchi takriban saba ambazo ni majirani zetu (Uganda, Rwanda, DRC Congo, Burundi, Zambia, na Malawi) na hivyo kuamua kuendelea kuutumia mfumo huu. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuendelea kuongezeka kwa kiwango cha mafuta yanayoagizwa na nchi hizo kupitia mfumo huu hapa nchini.

Kamati inaipongeza Wizara kwa kusimamia vyema uendeshwaji wa mfumo huu na kutoruhusu kuvurugika. Kamati inaendelea kusisitiza **kuwa, kama nchi tusiruhusu jambo lolote liuvuruge mfumo huu kwani kuvurugika kwake kunaweza kusababisha mafuta haya kuondoka kwenye mfumo wetu nchini na hivyo kupoteza faida za kiuchumi tunazopata kutokana na mafuta haya kupitia nchini. Aidha, Kamati inasisitiza kuwa, uwepo wa mafuta haya kwenye hifadhi za nchi yetu kunatuhakikishia uhahika wa kuwepo kwa mafuta nchini, hivyo kama Taifa tuna kilasababu ya kuhakikisha hatuipotezi faida hii.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuimarika kwa mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja na hivyo kuihakikishia nchi uhakika wa usalama na upatikanaji wa mafuta nchini, kuendelea kwa vita kati ya nchi za Urusi na Ukraine tangu mwezi Machi 202022 kumeifanya Dunia kushuhudia uwepo wa athari za kiuchumi zilizotokana na kuongezeka kwa bei za mafuta kwa kiwango kikubwa, na hivyo kusababisha kuwepo kwa changamoto ya upatikanaji wa Dola za Marekani. Hali hii imeleta athari kubwa katika biashara ya mafuta kwa nchi mbalimbali ulimwenguni ikiwemo nchi yetu. Kwa hapa nchini Kampuni za mafuta zimejikuta zikichelewa kulipia shehena zao za mafuta na hivyo shehena hizo kulazimika kubaki katika maghala ya mafuta chini ya uangalizi wa mletaji mafuta (*Financial Hold*) hadi pale yanapolipiwa. Hali hii ya mafuta kuwa kwenye maghala chini ya uangalizi imesababisha uhaba wa nafasi ya kupokelea shehena nyingine jambo ambalo linasababisha kupungua kwa ufanisi wa mfumo wa BPS.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuondokana na changamoto ya upatikanaji wa Dola za Marekani na hivyo shehena za mafuta kulazimika kubaki katika maghala chini ya uangalizi wa

mletaji, **Ni Rai ya Kamati kuwa Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania ione umuhimu wa kuongeza kiasi cha uuzaji wa Dola za Marekani katika soko. Aidha, katika kipindi hiki cha uhaba wa Dola za Marekani katika soko la ndani, mapitio ya haraka ya muongozo wa uendeshaji wa soko la fedha wa mwaka 2020 yanahitajika ili kuondoa vipengele vinavyokwamisha kufanyika kwa Inter-Bank foreign exchange (IFEM). Sambamba na hilo, Serikali ihakikishe kuwa mafuta yanayoenda nchi jirani yanalipiwa na nchi husika, na kwamba fedha zetu za kigeni zitumike kununulia bidhaa za nchi yetu tu ili kupunguza mzigo unaobebeshwa nchi yetu katika kulipia bidhaa za nchi jirani.**

*SEHEMU YA NNE*

## 4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi huo wa kina, Kamati inapenda kutoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo

### 4.1 Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania (TANESCO)

a) Ili kuepuka changamoto ya kuchelewa kutekelezwa kwa miradi kwa wakati kama ambavyo imebainika kwenye ukaguzi wa miradi, TANESCO inapaswa kuwa na Mkakati wa usimamizi wa Miradi (*Project Management*) ili kuwezesha miradi kukamilika kwa wakati na hivyo kuongeza uzalishaji wa umeme nchini;

b) Kutokana na deni la mauzo ya gesi kutoka TPDC kwenda TANESCO kuendelea kukua hadi kufikia **Shilingi Bilioni 720** ikilinganishwa na **Shilingi Bilioni 526** za Mwaka wa Fedha 2022/2023. N kwa kuwa licha ya ushauri wa mara kwa mara wa Kamati wa deni hili kulipwa hali inayozoretesha utendaji kazi wa TPDC, **Kamati inashauri Mwaka huu wa Fedha 2023/2024 deni hili lote lilipwe;**

c) Kumekuwa na utaratibu usiofaa wa baadhi ya Taasisi za Serikali kutolipa ankara za umeme hali ambayo imepelekea deni kufikia **Shilingi Bilioni 334.8.** Kwa mara nyingine **Kamati inashauri hatua za makusudi zichukuliwe ili deni hili lilipwe kabla ya Mwaka ujao wa Fedha 2023/2024 kuisha;**

d) Kutokana na baadhi ya maeneo nchini kutokuwa na umeme wa uhakika kutokana na ukosefu wa miundombiu isiyokidhi mahitaji kama vituo vya kupooza umeme (*Substation*) na Mashine umba (*Transfoma*), **TANESCO iboreshe miundombinu hiyo kwa kuharakisha ujenzi wa vituo vya kupooza umeme (*substations*) na kuweka mashine umba zinazoendana na mahitaji; na**

e) Kutokana na ari kubwa ambayo nchi inayo katika kutekeleza miradi mikubwa kama Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere, **Serikali ianze mradi mkubwa wa kuzalisha umeme kama huu kwa kutumia fedha zetu za ndani ili kuongeza uzalishaji wa umeme nchini.**

## 4.2 Wakala wa Umeme Vijijini –REA

a) Kutokana na utekelezaji usioridhisha wa miradi mingi ya REA. Uchunguzi wa kina (*Due Diligence*) ufanyike kabla ya kuwapa wakandarasi kazi;

b) Mkakati wa Serikali wa kutaka kuwasaidia Wakandarasi wa nje kwa kuwapatia dhamana (*Letter of Credit* - LC) ujielekeze kwa Wakandarasi wazawa ambao ni wazalendo ili kuwainua;

c) Vipengele vya Mkataba na Kampuni ya Tontan inayotekeleza Mradi wa Lot 39 viangaliwe na hatua kali zichukuliwe ili iwe fundisho kwa Wakandarasi wengine ambao wamekuwa wakisuasua kukamilisha miradi licha ya kupewa fedha; na

d) Pamoja na jitihada zinazofanywa na Wizara na Serikali katika kuhamasisha Nishati safi ya kupikia, Serikali katika Mipango yake iwezeshe matumizi ya majiko ya umeme yenye presha (*pressure cookers*) zinazotumia umeme kidogo pamoja na Mkaa mbadala unaotokana na makaa ya mawe (*Rafiki Coal Briquette*) ambao umethibitishwa kutokuwa na hewa/kemikali zinazosababisha uchafuzi wa mazingira na kuhatarisha afya za watumiaji. **Aidha, Serikali ione namna ya kupunguza kodi za uingizwaji wa majiko ya umeme yenye presha. Mkurugenzi wa Kimataifa wa Energy and Extractive Industries Riccardo Pulit amewahi kusema " *Clean cooking must be a political, economic and environmental priority, supported by policies and backed by investments and multi-sector partneship. To make that kind of change, the level of commitment and the scale of investment matter* "**

### 4.3 Shirika la Maendeleo la Petroli (TPDC)

a) Kamati imebaini kasi ya usambazaji wa gesi majumbani na kwenye Taasisi bado hairidhishi. Katika Mwaka huu wa fedha 2023/2024 Serikali imetenga **Shilingi Bilioni 20** kwa ajili ya kuunganisha wateja zaidi ya 1500. **Kamati inaitaka TPDC kuhakikisha lengo hili linafikiwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha Makampuni 20 ambayo yamepewa idhini ya ujenzi wa vituo vya kujazia gesi yanaanza ujenzi huo mara moja;**

b) Mahitaji ya gesi nchini yameongezeka ikilinganishwa na hali ya uzalishaji ilivyo. Kamati inatambua mpango wa Serikali wa kuendeleza vitalu kikiwemo Kitalu cha Ruvuma ambacho kina ugunduzi wa futi za ujazo **Trilioni 1.6** ambapo uzalishaji unatarajiwa kuanza na kiasi cha futi za ujazo **Milioni 40** kwa siku mwishoni mwa Mwaka 2023 na kufikia futi za ujazo **Milioni 140** mnamo mwaka 2027 pale uzalishaji utakapofikia kiwango cha juu. **Kamati inasisitiza uzalishaji katika Kitalu hiki uanze mapema na vitalu vingine ili kusaidia katika uzalishaji wa umeme nchini na matumizi mengine ya majumbani na viwandani;**

c) Tangu kuanzishwa kwa Mfuko wa Mapato ya Mafuta na Gesi kuanzia mwaka 2016/2017 kiasi cha **Shilingi Bilioni 342.34** zimekusanywa. Kamati inatambua nia ya Serikali ya kuhakikisha fedha hizi zinasaidia vizazi vijavyo, Hata hivyo, kutokana na nia ya kuendeleza miradi ya TPDC, **Kamati inashauri Serikali kuharakisha kuleta Marekebisho ya Sheria hii ili katika Mwaka huu wa fedha 2023/204 iweze kupitishwa na Bunge; na**

d) Kwa kuwa Kampuni Tanzu ya ya TANOIL ina umuhimu wa kimkakati katika biashara ya mafuta nchini. Kupitia ushiriki wake kwenye biashara hii kunaiwezesha Serikali kuwa na jicho la moja kwa moja na hivyo kuiwezesha nchi kuwa na udhibiti katika biashara hii ikiwemo kuzuia mbinu za wafanyabiashara wasiowaaminifu kupanga njama za kukwepa kodi au kufanya

makubaliano ya kupanga bei kwa lengo la kuua ushindani kwa manufaa yao. Ili TANOIL iweze kutimiza majukumu yake kikamilifu, **ipo haja kwa kampuni hii kupewa kila aina ya msaada unaohitajika Ili iweze kujiimarisha kwa kuwa na wafanyakazi wenye taaluma ya juu waliojengewa uwezo katika masuala ya biashara ya mafuta. Aidha, TANOIL iwezeshwe kimtaji ili iweze kujenga mtandao mpana na imara wa kibiashara hapa nchini; na hatimaye baada ya kujiimarisha iweze kuvuka mipaka na kufanya uwekezaji kwenye nchi jirani ambazo zinategemea bandari zetu kuingiza mafuta kwenye nchi zao.**

### 4.4 Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli - PURA

Kamati inarudia ushauri ilioutoa Mwaka 2022 kuhusu kuharakishwa kwa Mchakato wa kunadi Vitalu vilivyo wazi maeneo ya nchi kavu na baharini katika Duru ya Tano hasa ikizingatiwa kuwa mahitaji ya gesi nchini yameongezeka ikilinganishwa na hali ya uzalishaji ambayo ni ndogo.

### 4.5 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)

Jukumu la kuweka Vinasaba kwenye mafuta awali lilikuwa linatekelzwa na EWURA. Hata hivyo, baadae jukumu hili lilihamishiwa kwa TBS. kamati imebaini kuwa, kumekuwa na changamoto katika utekelezaji wa jukumu hili ikiwa ni pamoja na TBS kushindwa kutengeneza vinasaba vyake kama ilivyoshauriwa awali. Kamati inashauri:-

a) TBS iwezeshwe ili iweze kutengeneza vinasaba hivi na hivyo kusaidia kupunguza gharama katika bei ya mafuta; na

b) TBS iwezeshwe kwa kuwa na watumishi wa kutosha na vitendea kazi ili kuifanya kazi hii kwa weledi unaostahili.

## 4.6 Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA)

Kutokana na hatari inayoweza kutokea ya upungufu wa mafuta nchini kutokana na ukosefu wa dola za kimarekani nchini kwa ajili ya kulipia shehena za mafuta zinazoagizwa kutoka nje (*Financial Holding)*, Serikali ikiongozwa na Benki Kuu ichukue hatua za makusudi kuhakikisha nchi inakuwa salama.

## 4.7 Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania - TGDC

a) Joto ardhi ni rasilimali muhimu katika uzalishaji wa Umeme. Umeme unaozalishwa kwakutumia rasilimali hii huwa na gharama ya chini sana pindi uwekezaji wa awali unapokuwa umekamilika baada ya utafiti wa kina. Kwakuwa nchi yetu inayo rasilimali hii kwa wingi, Serikali iiwezeshe TGDC ili iweze kutimiza majukumu yake na hatimaye kuwezesha rasilimali ya Joto ardhi kuweza kutumika kuzalisha umeme wa uhakika na wa bei nafuu;

b) Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii na Sekta binafsi zione namna ya kuendeleza miradi mingine inayotokana na joto ardhi kama utalii, teknolojia ya utotoleshaji wa vifaranga kwa mashine(incubators); na

c) Sheria ya sasa inatambua rasilimali ya joto ardhi kuwa ni madini. Hata hivyo, matumizi makubwa ya joto ardhi ni katika umeme. mkanganyiko huu unasababisha wawekezaji kushindwa kuja kuwekeza. Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali ione umuhimu wa kuleta Sheria itakayowezesha rasilimali ya Joto ardhi kujulikana kama nishatii ili kusaidia kupata uwekezaji wa kutosha.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine napenda kuchukua fursa hii kukushukuru Spika wetu Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb) kwa uongozi wako thabiti. Pamoja nawe namshukuru sana Naibu Spika Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb) na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi imara wa unaowezesha utekelezaji mzuri wa majukumu yetu ya Kikatiba.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kwanza kwa heshima waliyonipa Mimi kuwa Mwenyekiti wa Kamati pamoja na mwenzangu Mhe, Judith Salvio Kapinga (Mb) kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Tunawaahidi ushirikiano wa kutosha katika kuisimamia Serikali. Aidha, tunawashukuru sana Wajumbe kwa kujitoa wakati wa ziara na wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Wizara hii. Taarifa hii ya Kamati ni juhudi za Wajumbe hawa ambao wana weledi mzuri katika Sekta hii ya Nishati kwa ujumla. Naomba kwa heshima wajumbe watambuliwe kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Judith Salvio Kapinga, Mb - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb
4. Mhe. Dkt. David Mathayo David, Mb
5. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb
6. Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb
7. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb
8. Mhe. Aleksia Asia Kamguna, Mb
9. Mhe. Kasalali Emmanuel Mageni, Mb
10. Mhe. Tabasamu Hamisi Mwagao, Mb

11. Mhe. Iddi Kassim Iddi, Mb
12. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb
13. Mhe. John Michael Sallu, Mb
14. Mhe. Juliana Didas Masaburi, Mb
15. Mhe. Maimuna Ahmad Pathan, Mb
16. Mhe. Masache Njelu Kasaka, Mb
17. Mhe. Ndaisaba George Ruhoro, Mb
18. Mhe. Nicodemas Henry Maganga, Mb
19. Mhe. Robert Chacha Maboto, Mb
20. Mhe. Saada Mansour Hussein, Mb
21. Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, Mb
22. Mhe. Martha Festo Mariki, Mb

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru sana Waziri wa Nishati Mhe. Januari Y. Makamba (Mb), Naibu Waziri Mhe. Stephen L. Byabato (Mb), Katibu Mkuu Eng. Felchesm Mramba, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Athuman Mbuttuka, pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Nishati kwa ufafanuzi na ushirikiano wanaoipa Kamati katika kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba wakati wote.

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru kipekee Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi (*ndc)* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto *(ndc*) , Makatibu wa Kamati yetu Ndg. Pamela Pallangyo, Ndg. Onesmo Laulau, Ndg. Jesca Sanga, Msaidizi wa Kamati Ndg. Rukia Shaban pamoja na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kutuhudumia wakati wote na kuchangia kukamilika kwa Taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati (**Fungu 58)** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.



Dunstan Luka Kitandula, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**

2023